# Hotuba ya Chuo Kikuu cha Al-Azhar katika Kazi ya Ufunguzi wa Ofisi ya Kanda ya Muungano wa Vyuo Vikuu vya Kiafrika Nchini Sudan

Namshukuru Mwenyezi Mungu, Sala na Salamu ziwe kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, na watu wake, Masahaba wake, na wale wote wenye kupita kwenye njia yake kwa ihsani mpaka Siku ya Kiyama.

Amani iwe kwenu na rehema za Mwenyezi Mungu na baraka zake…

**Waheshimiwa mliohudhuria!**

Mwanzo kabisa nakupeni salamu za Mheshimiwa Imamu Mkuu Sheikh wa Al-Azhar Prof. **Ahmad Al-Tayyib** na salamu za Prof. **Muhammad Hussein Al-Mahrasawi** Mkuu wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar ambapo wakimwomba Mwenyezi Mungu mpate taufiki kwa manufaa ya watu wote.

Nina furaha ya kutanguliza shukrani kwa Mkuu wa Muungano wa Vyuo Vikuu vya Kiafrika.

Shukrani kwa Prof. **Etienne Ehouan Ehile** – Katibu Mkuu wa Muungano wa Vyuo Vikuu vya Kiafrika, kwa kutualika kuhudhuria kazi za ufunguzi wa ofisi ya kanda ya Afrika Mashariki.

Kama vile tunatoa shukrani kwa Prof. **Ahmad Aly Suleiman** – Mkuu wa Chuo Kikuu cha Khartoum, kwa mapokezi mazuri na makaribisho, pia ninatoa pongezi kwa wananchi ndugu wa Sudan pamoja na Chuo Kikuu cha Khartoum kwa kuteuliwa kuwa makao makuu ya kudumu ya ofisi ya kanda ya Muungano wa Vyuo Vikuu vya Kiafrika kwa eneo la Afrika Mashariki, sisi tunatambua uteuzi huu, kwani chuo hiki kinastahiki kwa umbo lake na madhumuni yake jukumu hili, sisi tuna imani kubwa kuwa kitasimamia jukumu lake kwa ukamilifu na kitakuwa

na nafasi katika kuboresha elimu pamoja na kuhudumia jamii na kuendeleza mazingira ya Kiafrika.

Ukweli wa mambo ni kuwa, Muungano wa Vyuo Vikuu vya Kiafrika unafanya juhudi kubwa na ya wazi katika kuboresha elimu ya juu Barani Afrika, kama vile umekuwa na nafasi muhimu na yenye nguvu katika kupunguza mwanya kati ya Afrika na Ulaya katika masuala mbalimbali ya utamaduni, elimu na maarifa, kwa kuongeza pia uboreshaji wa ngazi za wahitimu na kuwajengea uwezo.

Chuo Kikuu cha Al-Azhar – kama mnavyofahamu waheshimiwa – umri wake ni miaka elfu moja na arubaini na nane, kinakusanya ndani yake programu 359 za kiakademi kwenye elimu mbalimbali na maarifa ya Kidini, kisayansi na kitiba, na Chuo Kikuu cha Al-Azhar kina matawi makuu matatu: la kwanza lipo Jijini Kairo, la pili: lipo Kusini mwa Misri na la tatu: lipo Kasikazini mwake. Chuo kina vitivo themanini na saba, na ndani ya mwaka wa (2017/2018) kinasomesha wanafunzi (kiasi cha laki 650000), pia kinasomesha wanafunzi wa kimataifa kiasi cha 33000, wakitokea nchi 107 duniani, miongoni mwao wanafunzi kutoka nchi 35 ni Afrika Kasikazini, Kusini, Mashariki, Magharibi na kati kati mwa Afrika, idadi yao jumla inafikia wanafunzi 6164.

Al-Azhar Al-Sharif kinatoa shime kubwa ya kushughulikia kazi mbalimbali kwa nchi zote za Afrika ndani ya nyakati tofauti, mfano kupeleka wajumbe wa kielimu katika elimu mbalimbali, maarifa na tamaduni, misafara ya madaktari na misaada ya kibanadamu kwenye maeneo yaliyotokewa na majanga, imefikia idadi 13 ya misafara ya madaktari kuanzia 2011 mpaka februari 2018 kwa nchi saba za Kiafrika nazo ni: (Sudan, Niger, Somalia, Chad, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Nigeria, na Burkina Faso) ambapo madaktari 124 walishiriki katika misafara ile na idadi ya wagonjwa ilifikia 61385 na idadi ya operesheni ilifikia 1430 na shehena za dawa zilifikia 17 tani. Ama ile misaada ya

kibinadamu, basi ilifikia nne mnamo miaka miwili kwa nchi za (Chad, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Nigeria na Somalia).

Kama vile Chuo Kikuu cha Al-Azhar Al-Sharif siku zote kinatoa shime kubwa ya kuingia mikataba na Vyuo Vikuu mbalimbali vya nchi za Afrika.

Al-Azhar Al-Sharif hufanya makongamano kwa maimamu wa misikiti na masheikh katika nchi mbalimbali za Kiafrika kwa kushirikiana na Kituo cha Tony Blair cha Kiingereza.

Al-Azhar imeanzisha Kituo cha Uchunguzi ili kupambana na siasa kali, na kutoa umuhimu mkubwa wa kueneza Dini iliyo sahihi na kupambana na vitendo vyote ambavyo vinadhuru kwa mwanadamu na viumbe vyengine pamoja na mazingira, kisha Al-Azhar inajibu siasa hizo na matendo hayo pamoja na kuyasahihisha kwa kutumia lugha kumi na moja, kama vile inatoa umuhimu kupambana na fikra za kigaidi ulimwenguni, na kutahadharisha vijana kutokana na fikra potofu, imekuwa pia na duru ya wazi katika kupambana na siasa kali na ugaidi ikitumia njia za elektroniki.

Muungano wa Vyuo Vikuu vya Kiafrika ndio upande unaohusika na kuweka mpango wa mkakati wa elimu ya juu Barani, kujenga mifumo bora ya elimu ili kudhamini ubora wa wahitimu na ushindani wao kwenye soko la Kimataifa la ajira.

**Waheshimiwa mliohudhuria!**

Mnafahamu kuwa mivutano na magomvi ya ndani ya Bara ni moja ya vikwazo vya maendeleo, hivyo huenda waheshimiwa mnaona umuhimu wa kuweka mkakati wa programu ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu – viongozi wa baadaye – ili kujenga misingi ya kuishi pamoja kwa amani na kuwakubali wengine, pamoja na mafunzo ya uwezo wa mawasiliano.

**Waheshimiwa mliohudhuria!**

Huenda mtashiriki rai na mimi katika umuhimu wa kupatikana chombo cha kujenga uwezo wa wana wa Bara la Afrika ili kushiriki katika kazi za maendeleo ya kudumu.

**Waheshimiwa mliohudhuria!**

Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi ulimwenguni, huenda baadhi ya nchi za Bara la Afrika ndani ya kipindi kijacho zikakumbwa na tatizo la ukame, jambo ambalo linapelekea kuwepo kwa haja kubwa ya kuwepo mifumo mbadala ya umwagiliaji maji isiyokuwa ile ya kijadi.

**Mheshimiwa Rais!**

Miongoni mwa changamoto za maendeleo Barani Afrika haiwezekani kusahau kadhia ya maradhi ya kudumu, ambayo yanapelekea matatizo ya kiuchumi na kukwamisha maendeleo, hivyo basi huenda mtashirikiana na mimi mawazo katika umuhimu wa kupewa uzito programu za akademi na tafiti za kisayansi ili kumaliza maradhi haya.

“Afrika” ni Bara tajiri zaidi duniani kwa vyanzo vyake asilia, hivyo ni lazima kugundua utajiri wake asilia na kudhamini uwekezaji wake mzuri kupitia programu ya akademi na tafiti za kisayansi.

“Mwanamke” ni mshirika mkubwa wa maendeleo ya kudumu ndani ya Bara la Afrika, hivyo ni lazima programu ya akademi na kazi za kitamaduni kuipa umuhimu nafasi ya mwanamke na umuhimu wake katika maendeleo ya kudumu na kujenga misingi ya usawa kati yake na mwanamume, na ubora ni kwa mwenye sifa ya pekee.

**Waheshimiwa mliohudhuria!**

Chuo Kikuu cha Al-Azhar kutokana na kuwa na uzoefu kinaweza kutoa mchango katika kuweka mikakati ya kiutendaji ya majukumu haya na utakelezaji wake.

**Mheshimiwa Rais!**

**Waheshimiwa mliohudhuria!**

Kwa jina la Al-Azhar Al-Sharif na Chuo Kikuu chake nawashukuru sana kwa mwaliko wenu na usikivu wenu, na ninamwomba Mwenyezi Mungu Atusaidie Tufanye kazi pamoja kwa manufaa ya watu wote katika kila zama na pahala.

Na mwisho wa wito wetu ni: "Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote"